# Matokeo yenye nguvu, Athari iliyothibitishwa

Kujifunza kidijitali kunakoleta matokeo yenye nguvu duniani kote

## MAELEZO YA JUMLA

Timu ya Enuma imejidhatiti kukuza elimu bora na yenye usawa ambapo kila anayejifunza atafanikiwa. Program yetu pana iliyoko kwenye mfumo wa tabuleti imeonyesha...

01 **Faida zinazoonekana kwenye kusoma kuandika na kuhesabu**

02 **Matokeo yaliyoboreshwa, kwa wale wanaoyahitaji zaidi**

03 **Faida zenye mabadiliko hata nje ya taaluma**

## 01 Faida ambazo hazijawahi kuonekana za kusoma, kuandika na kuhesabu: Kusaidia Lengo namba 4 la maendeleo endelevu (SDG4)

Matokeo kujifunza yenye nguvu yatolewa


### MAJARIBIO YALIYOFANYWA NA Global Learning XPRIZE

WANAFUNZI **450** | MIEZI **15** | **Tanga, Tanzania**


Kitkit Shule ni mojawapo wa washindi watano wa shindano linaloendelea la XPRIZE, linalofanywa na UNESCO pamoja na Shirika la Chakula duniani kutoka mwishoni mwa mwaka 2017 - 2019. Kitkit Shule ilipata matokeo makubwa zaidi kwenye washiriki wote waliofika fainali na matokeo yalikuwa makubwa ambayo hayajawahi kuonekana.

Matokeo ya kusoma, kuandika na hesabu yaliyopangwa kutokana na mazoezi madogo ya muda kutoka katika zana ya tathmini ya madaraja ya awali kwenye kusoma na hesabu(EGRA/EGMA), ilionyesha wastani wa matokeo ya wanafunzi waliotumia Kitkit yalikuwa na utofauti mkubwa ukilinganisha na ya wale ambao hawakutumia Kitkit.

**WASTANI WA MATOKEO YA KUSOMA NA KUANDIKA ULIONGEZEKA KWA MARA 4-5 ZAIDI**




**WASTANI WA MATOKEO YA HESABU ULIONGEZEKA KWA MARA 3-6 ZAIDI**





*Kujifunza zaidi, tafadhali soma muhtasari wetu wa kina wa Takwimu za GLXP.*

### UTAFITI ULIOFANYIKA 2017

WANAFUNZI **100** | MIEZI **3** | **Mtwara & Bagamoyo, Tanzania**

Majaribio yaliyodhibitiwa yameonyesha kwamba Kitkit shule ilikuwa na ufanisi katika kuboresha matokea yaliyotokana na kujifunza katika mazingira yote yakiwemo ya shuleni na yasiyo ya shuleni, Kujenga ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watoto katika makundi mawili ya majaribio: 1) miaka 6 hadi miaka 10 kwenye kituo cha jamii, 2) Kundi lililotumia Kitkit shule la wanafunzi wa kidato cha 1 hadi cha 3 katika shule ya msingi iliyopo katika mazingira ya kijijini




### UTAFITI ULIOFANYIKA 2018

WANAFUNZI **240** | MIEZI **3** | **Kaunti ya Turkana, Kenya**

Wanafunzi walioshiriki Kutumia Kitkit Shule walionyesha ongezeko kubwa katika matokeo ya majaribio yao ukilinganisha na ambao hawakutumia.

| | WALIOTUMIA KITKIT | WASIOTUMIA KITKIT |
|---|---|---|
| ONGEZEKO KWENYE KUSOMA NA KUANDIKA | ↑ 30 - 45% | - |
| ONGEZEKO KWENYE KUHESABU | ↑ 14 - 37% | ↑ 4 - 8% |

*Wanafunzi ambao hawakutumia Kitkit walionyesha mabadiliko madogo au hawakuonyesha kabisa katika majaribio yao.*

**UNGANA NASI**

Wasiliana nasi kwenye **kitkit@enuma.com** kujifunza zaidi kuhusu Kitkit shule, matokeo ya ukuaji wetu, na kujadiliana kuhusu fursa za kushirikiana

www.kitkitschool.com
kitkit@enuma.com
facebook.com/kitkitschool
twitter.com/kitkitschool

## 02 Kuongeza USAWA na UPATIKANAJI


Ushahidi kwamba Kitkit inasaidia wanafunzi WOTE, hasa hasa makundi ya walioachwa

### MATOKEO YA NGUVU KWA WAKIMBIZI

WANAFUNZI **240** | MIEZI **3** | **Kaunti ya Turkana, Kenya**

Mradi wa Xavier ulishirikiana na Enuma kuongeza upatikanaji wa elimu bora kwa wakimbizi na watoto walioko katika jamii inayokaa nao kwa kutumia Kitkit Shule. Kwa wanafunzi 35 waliochaguliwa bila mpangilio maalum, matokeo yalionyesha kuwa makubwa... hasa hasa kwa wale waliohitaji zaidi.

**Wimbi linalokua kwenye kambi ya wakimbizi ya Kakuma**
Matokea kabla na baada ya uchunguzi(Hesabu)




**Angalizo: Kila kidoti kinawakilisha utambulisho wa kipekee wa mwanafunzi*

## 03 Kuwawezesha wanaojifunza Kidijitali

Faida zenye mabadiliko kwa mtumiaji na jamii hata nje ya taaluma

### MOTISHA NA UFANISI BINAFSI

Katika taarifa ya mradi wa Xavier, timu yetu ya utekelezaji ilitoa taarifa jinsi kijana mdogo wa kiume ambaye alikuwa anapata shida kwenye mahudhurio na kwenye taaluma alianza kuwa mdadisi, mwenye maamuzi na mwenye hamu ya kujifunza.

"Toka hapo Nashim amekuwa mwanachama hai wa darasa la Kitkit.. **Kitkit Shule imempa motisha ya kuja shuleni kila siku** (Uk. 13)"

### USHIRIKIANO WA MUDA MREFU



Hatua ya kwanza kabisa ya kujifunza ni kumshirikisha mwanafunzi...



**Kwa kipindi chote cha shindano la global learning XPRIZE, wanafunzi waliotumia Kitkit Shule walikuwa na wastani wa masaa 285 kwa kila mwanafunzi.**

### UJUZI WA KIDIJITALI NA KUJITEGEMEA

Walimu kutoka Kigali, Rwanda walishangazwa sana na wanafunzi wao 44 wa shule ya awali ambao walijua namna ya kutumia tabuleti kwa haraka na kuanza kujifunza ndani ya dakika 30!

"Nilishangazwa. **Wanafunzi walithibitisha kuwa wana uwezo wa asili wa kujifunza vitu wenyewe**"
- Heeju, Mwalimu

Kitkit shule ilianzishwa kwa msaada wa ukarimu kutoka Shirika la ushirikiano la Korea(KOICA) mpango wa teknolojia ya ubunifu(CTS). Hadithi yetu ya athari isingewezekana kuwepo bila msaada wa washirika wetu

KOICA Korea International Cooperation Agency | Good Neighbors | XAVIER PROJECT | GLOBAL LEARNING XPRIZE EMPOWERING YOUNG MINDS EVERYWHERE



© 2019 Enuma, Inc. | Wasiliana nasi kwenye Kitkit@enuma.com